*Kioo cha Lugha, Juz. 22(1), 1-19*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v22i1.1

# Usukuku wa Ukolonia katika Mjadala wa Lugha ya Kufundishia nchini Tanzania

*Gervas A. Kawonga*[1]

## Ikisiri

Makala hii inahusu usukuku wa ukolonia unaotawala fikra za wasomi katika mjadala wa lugha ya kufundishia nchini Tanzania. Lengo lake ni kueleza kwa nini mapendekezo ya kubadilisha lugha ya kufundishia kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili yanapata ukinzani miongoni mwa wasomi nchini Tanzania. Data zilitokana na maoni ya wasomi kupitia kundi la *WhatsApp* la UDASA-MUCE. Kiunzi cha Ubadaukoloni kinachohoji ukamilifu wa ukombozi uliopatikana katika nchi nyingi zilizowahi kutawaliwa kimetumika kuongoza utafiti huu. Matokeo yanaonesha kwamba kuna usukuku wa ukolonia miongoni mwa wanazuoni unaoathiri fikra zao kuhusu lugha ya kufundishia licha ya juhudi za kuwazindua. Kwa hiyo, ukombozi dhidi ya ukolonia wa maarifa hasa miongoni mwa wasomi ni muhimu na ni suala linalopaswa kushughulikiwa kwa hatua za dharura ili kunusuru ubora wa elimu nchini Tanzania. Pendekezo ni kwamba serikali itumie madokezo ya sera yanayotokana na tafiti za kisayansi kwa ajili ya kufanya maamuzi kuhusu lugha katika elimu.

## 1.0 Utangulizi

Licha ya mapendekezo ya tafiti za kitaalamu kudhihirisha kwamba wanafunzi wanaweza kushiriki michakato ya ujifunzaji na uundaji wa dhana vizuri zaidi kwa kutumia lugha wanayoimudu vyema (Qorro, 2013; Telli, 2014; Vuzo, 2018; Kazeen na Suleiman, 2020), mfumo wa elimu nchini Tanzania bado unatumia lugha ya kigeni kufundishia. Kiingereza kinatumika kufundishia elimu ya msingi katika baadhi ya shule za serikali na binafsi, sekondari na elimu ya juu. Kiswahili kinatumika kufundishia elimu ya msingi katika shule nyingi za serikali na elimu ya juu kwa taaluma za Kiswahili peke yake (Kawonga, 2023). Vilevile, Kiswahili kinafundishwa kama somo katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia. Kwa mujibu wa Vuzo (2018), matumizi ya lugha ya kigeni katika

[1] Mhadhiri, Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Iringa Tanzania: Baruapepe: gervas.kawonga@udsm.ac.tz

elimu yanachangia kushusha ubora wa elimu na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi kukatisha masomo ya sekondari. Suala la wanafunzi kukatisha masomo linachochewa na kutoshirikishwa kikamilifu katika ujifunzaji kwa kutoimudu vyema lugha inayotumika darasani. Utafiti wa Qorro (2009) unahoji msimamo wa wazazi na watungasera kung'ang'ania matumizi ya lugha ya kigeni kufundishia ngazi zote za elimu ni kwa manufaa ya nani. Anafafanua kuwa tafiti zimeweka bayana kuwa walimu na wanafunzi nchini Tanzania hawaimudu lugha ya Kiingereza.

Senkoro (2008) anaeleza kuwa vitengo vya uthibiti ubora katika taasisi za elimu ya juu pamoja na masuala mengine, vinasisitiza matumizi ya lugha inayokubalika kwa mujibu wa Sera ya Elimu. Hairuhusiwi kutumia Kiswahili katika kozi ambazo zinapaswa kufundishwa kwa Kiingereza. Ingawa Sera ya Utamaduni ya Tanzania (1997) inaelekeza matumizi ya Kiingereza kuwa lugha ya kufundishia nchini Tanzania, utekelezaji wake haujafanikiwa kwa sababu walimu wanachanganya na kubadilisha misimbo kati ya Kiingereza na Kiswahili katika jitihada za kujieleza na kuwasaidia wanafunzi kuelewa maudhui muhimu ya somo husika (Mtallo, 2015). Hoja hiyo inaungwa mkono na Mutembei (2023) anapoeleza kwamba walimu wengi wanatumia Kiswahili kufundishia sekondari na hata vyuoni licha ya ukweli huo kuwa hautarajiwi kuelezwa kwenye vikao rasmi. Hali hiyo ni kiashiria kwamba kuna changamoto ya lugha ya kufundishia elimu ya sekondari na ya juu kwa walimu na wanafunzi. Kwa nini Sera ya Elimu bado inasisitiza matumizi ya lugha ya kigeni katika elimu ya Tanzania licha ya ushauri unaotokana na tafiti?

Kunaweza kuwa na nadhariatete nyingi katika kujibu swali la kwa nini wazazi na watungasera wanaendelea kusisitiza Kiingereza kitumike. Mielekeo miwili inatajwa katika makala hii kwa minajili ya kujenga usuli wa makala yenyewe. Kwanza, inaelekea watungasera hawaongozwi na madokezo ya sera yanayotokana na tafiti za kisayansi kuhusu lugha na elimu. Fussy (2022) anatahadharisha kuwa kuna pengo baina ya watafiti na watungasera linalohitaji kuondolewa kwa hatua za dharura. Hata hivyo, mwelekeo huu unaweza kukosolewa kwa kutumia Kiunzi cha Ubadaukoloni kinachoongoza makala hii.

Pili, inaelekea watungasera wanafumbia macho matokeo ya tafiti kutokana na nguvu za kibeberu ambazo zimeathiri fikra za kujitegemea katika nchi zinazoendelea ikiwa ni pamoja na kukosa uhuru wa kuchagua lugha ya kurithisha amali zake. Nadhariatete hii ya pili inapewa nafasi kubwa kutokana na mwangwi wa ukolonia unaodhihirika katika maoni ya wasomi ambayo ni data za utafiti huu. Kuna nguvu kinzani inayoathiri maamuzi kuhusu lugha katika elimu sawasawa na vipengele vingine vya kiuchumi na kiutamaduni. Nguvu kinzani inayoathiri maamuzi hayo, msingi wake wa ufafanuzi umewekwa bayana katika kiunzi cha Ubadaukoloni na kwa kutumia dhana ya ukolonia.

Pamoja na mjadala wa lugha ya kufundishia, kuna madai ya kushuka kwa ubora wa elimu nchini Tanzania. Mosha (2012) anaeleza kwamba elimu ya

Tanzania ipo kwenye janga kubwa licha ya mafanikio machache yanayoweza kuoneshwa hasa katika uandikishaji. Ochieng na Yeonsung (2021) wanaeleza kwamba Tanzania imepata mafanikio makubwa katika uandikishaji wa wanafunzi kupita kiwango cha wastani katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hata hivyo, wanatanabahisha kuwa udhaifu mkubwa wa elimu yake upo katika ubora. Elimu bora kwa mujibu wa Benki ya Dunia, inafumbatwa na kiunzi chenye vigezo sita. Vigezo hivyo ni: kutathminika, uhuru wa kuamua, uwajibikaji, ubora wa mwalimu, uzingatiaji wa makuzi ya awali ya mtoto na uzingatiaji wa utamaduni (World Bank, 2014). Kwa mujibu wa Fanon (2008) kama alivyonukuliwa na Mutembei (2023), elimu bora inahusishwa na ukuzaji wa fikra tunduizi kwa kujenga uwezo wa kujieleza, kutathmini mambo, kufikiria jambo linaloweza kutokea kutokana na uamuzi wa sasa, kufahamu changamoto na kuzitatua na uwezo wa kujenga hoja. Uzingatiaji wa utamaduni (World Bank, 2014) unahusisha matumizi ya lugha mama au lugha inayofahamika vizuri kwa jamii, walimu na wanafunzi. Hii ni nguzo muhimu pia katika kukuza fikra tunduizi. Faida ya matumizi ya lugha ya mawasiliano mapana ya jamii husaidia pia kuongeza mahudhurio, kupunguza wanaorudia na wanaokatisha masomo, hivyo, kuongeza ubora wa elimu (Ochieng na Yeonsung, 2021). Miundombinu ni suala linalofuatia kwa vipaumbele vya kutoa elimu bora kwa mujibu wa kiunzi cha Benki ya Dunia.

Kwa hiyo, kwa kuwa Tanzania inatumia lugha ya kigeni kufundishia badala ya Kiswahili ambacho kinafahamika na wengi, hiyo ni sababu mojawapo ya kushuka kwa ubora wa elimu nchini. Msisitizo wa Ochieng na Yeonsung (2021) ni kwamba kushuka kwa ubora wa elimu ya Tanzania kunatokana na sera ya elimu kutozingatia vigezo vya ubora vilivyowekwa na Benki ya Dunia. Kwa maneno mengine, utamaduni wa jamii haujazingatiwa sawasawa katika mfumo wa elimu ya Tanzania. Brock-Utne (2015) anasisitiza kwamba tatizo kubwa la ujifunzaji kwa watoto wa Kiafrika ni la kiisimu linalosabishwa na matumizi ya lugha za kigeni. Kutumia lugha ya kigeni kunaifanya dhana ya elimu kwa wote kuwa mchakato usiokamilika kwa ufanisi stahiki. Maelezo hayo yanaelekeana na msisitizo wa Meena (2023) kwamba mabadiliko ya lugha katika ngazi ya sekondari yana athari hasi kwa wanafunzi ambao wanakuwa wamehitimu shule za msingi ambazo hazitumii lugha ya Kiingereza kufundishia.

Huku kukiwa na mjadala wa muda mrefu kuhusu lugha ya kufundishia, tarehe 25 Julai, 2022 Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alieleza mpango wa serikali wa kuandaa mitaala mipya na kufanya mapitio ya Sera ya Elimu kwa ajili ya kuboresha elimu nchini Tanzania. Waziri alieleza hayo katika Mkutano wa Kikosikazi cha Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya elimu duniani uliofanyika mkoani Kilimanjaro (Lymo, 2022). Hatua hiyo ya serikali inafuatia malalamiko ya zaidi ya miongo minne ya kushuka kwa ubora wa elimu nchini Tanzania (Makweta, 2012). Kwa mujibu wa Meena (2023),

kila matokeo ya mtihani wa upimaji au wa taifa yanapotolewa, mjadala wa lugha ya kufundishia unaibuka. Pamoja na mantiki hiyo, mchakato wa mapitio ya mitaala ya elimu unaendeleza zaidi mjadala kuhusu lugha ya kufundishia. Hii inatokana na msisitizo kwamba miongoni mwa vigezo muhimu katika kuinua ubora wa elimu, lugha ya kufundishia inachukua nafasi muhimu zaidi. Mjadala kuhusu lugha ya kufundishia unahitaji weledi kwa sababu ni suala changamani ambalo linahitaji uangalifu kulitolea maoni yanayoweza kueleza msingi wa changamoto na kupendekeza suluhisho lenye mustakabali stahiki kwa taifa. Hata hivyo, masuala mengine kama vile miundombinu, ubora na idadi ya walimu, pamoja na vifaa vya kujifunzia na kufundishia ni ya lazima katika kuinua ubora wa elimu na haviwezi kupuuzwa.

Kabla ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kutangaza mpango wa serikali tarehe 10 Juni 2022, lilifanyika kongamano katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhusu lugha ya kufundishia shuleni. Kongamano hilo lilifuatiliwa na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wasomi wa Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa. Ufuatiliaji wa wanazuoni hao, uliibua mjadala mkubwa wa maandishi katika kundi la *WhatsApp* linalojulikana kwa jina la UDASA-MUCE. UDASA ni kifupisho cha maneno ya lugha ya Kiingereza yanayomaanisha Jumuiya ya Wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa upande mwingine, MUCE ni kifupisho cha jina la Kiingereza la Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa ambacho ni Chuo Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mjadala huo wa wanazuoni ni kichokoo kilichomfanya mwandishi afikirie mada kuhusu usukuku wa ukolonia katika mjadala wa lugha ya kufundishia nchini Tanzania.

Usukuku ni sitiari iliyojengwa kwenye misingi ya kiakiolojia yenye maana ya hali ya masalia ya vitu au wanyama katika kiwango cha mwisho cha kutobadilika tena kikemia baada ya miaka mingi kupita. Katika makala hii dhana ya usukuku inamaanisha hali ya wasomi kuendelea na fikra za kikoloni kiasi cha kushindwa kubadilika licha ya juhudi zinazofanyika kuwazindua. Kwa upande mwingine, ukolonia ni ugonjwa wa kisaikolojia unaozuia fikra razini katika kipindi cha baada ya ukoloni kwenye jamii zilizotawaliwa. Ugonjwa huo hufanya mtu ajitathmini kwa kutumia maadili na vigezo vilivyowekwa na tamaduni za watawala wake wa zamani (Bokamba, 2011) na kujidharau yeye mwenyewe. Dhana zote mbili zimetumika kuonesha jinsi urazini wa washiriki wa mjadala wa lugha katika elimu ulivyotekwa nyara na fikra za kikoloni na kushindwa kulisaidia taifa kuamua kwa usahihi kuhusu lugha ya kufundishia. Kuhusiana na dhana hizo zote mbili kwa muktadha wa makala hii, kuna maoni mengine kwamba:

> …inatarajiwa kuwa msomi anajua uhusiano baina ya lugha na elimu au tuseme lugha na ujenzi wa maarifa, anatarajiwa kujua kuwa ufundishaji wa lugha ya kigeni kama somo na lugha inayotumika kufundishia ni mambo mawili tofauti. Ikiwa hajui, kuna tatizo katika kusoma kwake.
>
> **Chanzo:** Mutembei (2023: 17)

Wasiounga mkono kuwapo kwa tatizo la kusoma kwa wasomi kama inavyodokezwa kwenye dondoo la hapo juu, wanaweza kuwa na utetezi rahisi kwamba kinachotajwa kuwa ni udhaifu si udhaifu bali ni mtazamo wao na hautokani na tatizo katika kusoma kwao, hivyo, unafaa kuheshimiwa. Licha ya uhuru huo wa maoni, makala hii ina mtazamo kwamba hilo linaloonekana kuwa ni tatizo la kusoma kwa wasomi, ni matokeo ya ukolonia unaowafanya wautazame ulimwengu na kuiona hali halisi kwa kutumia lugha na utamaduni wa kigeni kama inavyoelezwa katika sehemu ya uwasilishaji wa matokeo ya utafiti huu.

## 2.0 Methodolojia na Kiunzi cha Kinadharia

Utafiti huu ni wa kitaamuli ambao data zake zilitokana na maoni ya wanazuoni katika mjadala ulioibuka kwenye kundi sogozi la *WhatsApp* la UDASA-MUCE tarehe 10 Juni, 2022. Mjadala huo ulichochewa na kongamano la lugha ya kufundishia shuleni lililofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tarehe 10 Juni, 2022 na kurushwa mubashara kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Matini 30 zilikusanywa na kufanyiwa uchambuzi wa kimaudhui. Kwa kuwa maoni yalitolewa kwa lugha ya Kiswahili, maneno au tungo za Kiingereza zilizochopekwa kupitia uchanganyaji na ubadilishaji msimbo zimetafsiriwa kwa Kiswahili katika mabano mraba ili kuendana na lugha kienzo ya makala hii. Jumla ya mada ndogondogo sita zimeibuliwa na kuwasilisha nukuu za matini mahususi kama data zinazoshadidia maudhui husika. Ufafanuzi wa kinathari umefanyika kuhakiki maudhui yaliyotokana na maoni ya wanazuoni walioshiriki mjadala huo kwa njia ya maandishi. Katika kuzingatia masuala ya itikeli, majina ya wachangiaji yamehifadhiwa. Uwasilishaji wa data unaenda sanjari na mjadala ili kupata muunganiko wenye ushikamani na kurahisisha uelewekaji wa hoja na data kwa msomaji. Katika hatua hii, ni suala muhimu kufafanua kiunzi cha Ubadaukoloni kinachoongoza utafiti huu.

### 2.1 Kiunzi cha Kinadharia

Makala hii imeongozwa na kiunzi cha Ubadaukoloni kinachokosoa hali ya mambo katika nchi zilizokuwa makoloni ya Ulaya hususani Afrika, Asia na Karibiani. Hivyo, ni sehemu ya mapambano dhidi ya masalia ya ukoloni mkongwe, ukoloni mamboleo na athari hasi za utandawazi. Msingi mkuu wa kiunzi hicho unatokana na mawazo ya wanazuoni mbalimbali (Fanon, 1952, 1961; Said, 1978; Ngugi, 1986) wenye nia ya kutetea kuwapo kwa mtu mweusi kiontolojia na kukataa kaida na mifumo inayobagua watu katika makundi kwa misingi ya rangi, umaskini, utamaduni, lugha na kila aina ya tofauti zinazoweka darajia msonge za watu bora na watu duni. Kiunzi hiki kinahoji jinsi maarifa ya Kimagharibi kuhusu mbari zilizokandamizwa yanavyozalishwa na kuenezwa. Msisitizo wake ni kwamba fikra katika makoloni ya zamani bado zinatawaliwa na mifumo ya kikoloni, hivyo,

ukombozi mwingine unahitajika kwa hatua za dharura ili utambulisho wa mtu mweusi udumishwe na kuheshimiwa.

Mkazo mkubwa wa harakati za ukombozi kamili unawekwa kwenye ukombozi wa fikra. Katika hali hiyo, kutumia lugha ya kigeni katika fasihi, elimu na shughuli zingine baada ya uhuru ni kielelezo cha kutekwa kifikra na kiutamaduni, hivyo, kumfanya mtu mweusi ajidharau na kujikataa. Ubadaukoloni unakataa kutawaliwa kilugha kutokana na lugha ya tabaka lenye nguvu kujiundia taswira dhahania ya ubora usio na kifani na kuahidi mafanikio kwa watakaoimudu. Lugha zinazotawaliwa hutwezwa, hukandamizwa na kunyanyapaliwa kwa madai kwamba haziwezi kuchangia chochote katika maendeleo na maarifa; ni mali ya lugha za tabaka lenye nguvu. Kwa jumla, kiunzi cha Ubadaukoloni ni mwafaka katika kueleza kwa nini jamii ya wasomi haitaki kuacha kutumia lugha ya kigeni shuleni.

## 3.0 Matokeo ya Utafiti na Mjadala

Sehemu hii inahusu matokeo ya uwasilishaji wa data na mjadala unaolenga kuonesha data husika ina maana gani katika muktadha wa utafiti huu. Uwasilishaji umefanyika kwa kuzingatia maudhui kuhusu nafasi ya lugha katika kuinua ubora wa elimu nchini Tanzania. Maudhui hayo yameainishwa katika makundi sita kama yanavyowasilishwa katika sehemu ya 4.1 hadi 4.6. Mjadala umefanyika kinathari katika kuonesha tajiriba iliyozaa fikra zinazojitokeza kupitia maoni ya wanazuoni na msingi wake katika kiunzi cha Ubadaukoloni.

### 3.1 Uhusiano wa Ubora wa Elimu na Lugha ya Kufundishia

Baadhi ya wanazuoni walionesha msimamo kwamba ubora wa elimu hauathiriwi na lugha inayotumika kufundishia. Mtazamo huu umejengwa katika hoja kwamba kuna baadhi ya wahitimu wa elimu ya msingi hawana stadi za kusoma na kuandika licha ya lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia katika ngazi hiyo ya elimu. Mchangiaji mmojawapo aliandika:

> Sasa we utashangaa watoto kuanzia la kwanza hadi la saba wanafundishwa Kiswahili masomo yote labda la Kiingreza chenyewe lakini bado kuna watoto wanamaliza bila kujua kusoma na kuandika *yet* [bado] kuna mtu anaamini mwarobaini wa matatizo yetu ya elimu ni Kiswahili.
>
> **Chanzo:** *WhatsApp* UDASA-MUCE, tarehe 10 Juni 2022

Maoni hayo yaliungwa mkono na mchangiaji mwingine wakati akijaribu kuelezea jinsi ambavyo huko Ukerewe wanafunzi wanafaulishwa kwa upendeleo. Madai yake ni kwamba wanafunzi walikuwa wanafundishwa kwa lugha ya Kiswahili na kufaulishwa mtihani ilimradi madarasa ya sekondari yapate wanafunzi licha ya kutojua kusoma na kuandika, mchangiaji huyo alieleza:

> ….. huko Ukerewe watoto wa *primary* [elimu ya msingi] walifaulishwa kwa sababu madarasa ya sekondari yalikuwa yamejengwa, hivyo yangekosa wanafunzi. Wamefika *Secondary* [sekondari] hawajui hata kusoma na kuandika kwa Kiswahili. Tuna safari ndefu sana.
>
> **Chanzo:** *WhatsApp* UDASA-MUCE, tarehe 10 Juni 2022

Madai kuhusu kilichotokea Ukerewe katika maelezo hayo ni mazito; yanahitaji kuhakikiwa usahihi wake kabla ya kuchukuliwa kuwa ni suala lililotokea kweli au ni maelezo yaliyotiwa chuku. Hata hivyo, jambo dhahiri ni kwamba wachangiaji wote wawili wanaelekea kupotosha mjadala kuhusu uwezekano wa kubadili lugha ya kufundishia kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. Mapendekezo ya tafiti hayaoneshi kwamba kubadili lugha ya kufundishia ni hatua pekee ya kuinua ubora wa elimu nchini Tanzania. Tafiti zinatambua kuwa miundombinu na rasilimaliwatu ni masuala ambayo lazima yashughulikiwe sambamba na suala la lugha ya kufundishia. Msisitizo unaopaswa kueleweka vizuri ni kwamba kuboresha miundombinu wakati walimu na wanafunzi hawaelewani darasani hakuwezi kuinua ubora wa elimu. Uelewa kuhusu uhusiano baina ya ubora wa elimu na lugha ya kufundishia, ulibainika kuwa mdogo miongoni mwa wachangiaji wengi. Hilo linajidhihirisha kwa mchangiaji mwingine anayeeleza:

> …ila *language* [lugha] mnaisingizia haimo.... wewe umemaliza PhD hapa unataka kuniambia hizo hesabu hauzijui ulizosoma, na zimefundishwa kwa lugha gani? Na ulisoma kikorea muda gani. Anaejifichia kwenye *language* [lugha] atafute sababu nyingine. Tuboreshe mazingira ya kujifunzia, walimu n.k ndo ufuate mjadala wa lugha. Wanafunzi wanafundishwa *titration theoretically* [kinadharia], *telescope* [teleskopu] kwa picha alafu unawalaumu kwa nini hawavumbui?
>
> **Chanzo:** *WhatsApp* UDASA-MUCE, tarehe 10 Juni 2022

Kutamalaki kwa mawazo kama hayo kwa kiasi kikubwa kunatokana na kile anachokiita Moshi (2023) ulimbukeni wa kupenda vya nje kuliko vya ndani. Kwa upande mwingine, hii inaashiria kile ambacho Mutembei (2023) anakiita unafiki na usaliti wa wasomi kwa kuwa wanatarajiwa kujua uhusiano uliopo baina ya lugha na uzalishaji wa maarifa. Kwa kigezo cha kiunzi kinachoongoza utafiti huu, kutamalaki kwa fikra hizo ni zao la usukuku wa ukolonia na kutawaliwa kiisimu na kiutamaduni. Hamza (2022) anaeleza kwamba kuna kazi kubwa inayopaswa kufanyika ili kuondoa utawala wa lugha za Kimagharibi zinazotumika kuufanya mfumo wa elimu na utamaduni uwe wa kigeni miongoni mwa nchi zilizotawaliwa.

Mtazamo huo ni sawa na ule wa Naragarajan (2006) kwamba wakoloni wamefanikiwa kuitukuza lugha yao na kujijengea ukuu usio na kifani huku ikitumika kujenga udhalili kwa watawaliwa ambao pia wameikubali hali hiyo.

Hoja kwamba kubadili lugha kunachukuliwa kuwa mwarobaini ni mtazamo ambao umetamalaki miongoni mwa wasomi. Fikra hizo hazina urazini makini kutokana na kukingwa na mifumo isiyoruhusu uhuru wa kufasili upya ulimwengu na hali halisi nje ya minyororo ya ukoloni. Maelezo haya yanaelekeana na yale ya Ngugi (1987) kwamba matumizi ya lugha za kigeni katika mitaala ya elimu yanapindua uhalisia - kichwa chini miguu juu, hivyo, kukwamisha ubunifu. Kundi la wasomi linaongoza katika kudhoofisha harakati za kutaka lugha za Kiafrika kama kilivyo Kiswahili kitumike kufundishia ngazi zote za elimu.

Kuchukulia kwamba uvumbuzi unategemea miundombinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia bila lugha stahiki ni suala linalopingana na tafiti za wabobezi wa lugha na elimu ambazo zimefanyika ndani na nje ya Tanzania (Meissner, 2008). Maoni mengine ya kutweza nafasi ya lugha katika kuinua ubora wa elimu yaliandikwa:

> Kimsingi, mimi nafikiri kama kuna mtu/watu wanafikiri elimu yetu inadumaa au hatuendelei kwa sababu ya kufundisha kwa Kingereza basi wanatudanganya tuu. Hata hivyo, ikiwa tunaamua kufundisha kwa lugha ya Kiswahili basi tuamue tu lakini sio kwa kisingizio kwamba eti hatuwezi kufikiri vizuri kisa lugha ya kufundishia.
>
> **Chanzo:** *WhatsApp* UDASA-MUCE, tarehe 10 Juni 2022

Kichocheo kikubwa cha fikra hizo ni usukuku wa ukolonia wa maarifa unaomfanya mtu ajione anaweza sawasawa na mtawala wake, suala ambalo haliwezekani. Ugumu wa kuimudu lugha ya kigeni umeelezwa na Mutembei (2023) kwamba gogo haliwezi kugeuka mamba hata likikaa majini kwa miaka mia moja. Ubaya wa maoni yaliyotolewa kwenye nukuu ya hapo juu ni kutumiwa na watungasera na kuhalalisha maamuzi yao kwa madai kwamba wamezingatia maoni ya wasomi. Maoni yanayotokana na athari za ukolonia wa maarifa yanachangia maamuzi yasiyofaa kuhusu lugha ya kufundishia. Phillipson (1997) ameeleza bayana kuwa vinara wa utungaji wa sera katika nchi zilizotawaliwa ni wataalamu kutoka nchi zilizotawala na wasomi wa nchi husika. Kuna ushahidi kuwa binadamu hufikiria vizuri zaidi kwa kutumia lugha anayoifahamu vizuri (Meissner, 2008; Mutembei, 2023) badala ya kujifariji kwamba inawezekana kuwa na fikra sahihi sawasawa na wazawa wa lugha za kigeni. Kimsingi, lugha ya kufundishia inapaswa kuwa kwenye kitovu cha mchakato wa kuboresha mitaala ya elimu nchini kwa sababu msingi wa ujifunzaji na ufundishaji ni mawasiliano yenye ufanisi baina ya wanafunzi na walimu.

### 3.2 Lugha ya Kimataifa Sharti Itumike Kufundishia

Sehemu hii inahusu maudhui yanayosisitiza kwamba Kiingereza ni lugha ya ulimwengu mzima ambayo ni lazima ifahamike kwa wahusika ili kuwa sehemu ya ulimwengu. Mtazamo huu unadai kwamba kutumia lugha ya kigeni kufundishia ni

kuongeza fursa kwa wajifunzaji kutumia lugha hiyo na kuimudu kama ilivyoelezwa na mchangiaji mmojawapo:

> Hii *issue* [hili suala] ya *internationalization* [umataifishaji] msiichukulie poa. Tujifunze ambacho hatujui. Kiswahili tunachotaka ni cha mawasiliano ambacho tayari tunacho, na si kuwa Kiswahili *professionals* [wataalamu]. *We are not isolated from the rest of the world* [sisi hatujajitenga na ulimwengu] wao [nchi za kigeni] wanapigana kujua Kiswahili ili wa-*capture the missed part* [watawale sehemu iliyobakia] ili wawe *efficient* [na ufanisi] kwenye *international trade and other international interactions* […biashara za kimataifa na mahusino mengine]. Itafika mahali Kiswahili tutakuwa hatujui wala Kiingereza tutakuwa hatujui. Kuna siku watatuzidi kila kitu, Kiswahili na Kiingereza. Tutashindwa kuomba kwa Kiswahili na pia kwa Kiingereza. Huko Kenya inafahamika na wanafundisha Kiswahili kuliko sisi waasisi. *My take* [mwelekeo wangu]; tujifunze vyote na mkazo uwe kwenye ambacho hatukijui [yaani mkazo kwenye Kiingereza].
> **Chanzo:** *WhatsApp* UDASA-MUCE, tarehe 10 Juni 2022

Maoni hayo yamejikita katika kuweka msisitizo wa kujifunza Kiingereza ili kutokujitenga na dunia na kwamba kutumia kufundishia kunaongeza nafasi ya wanafunzi kuimudu lugha hiyo. Kimsingi, huu ni usukuku wa ukolonia wa maarifa ambao unapaswa kuteketezwa na kuleta ukombozi wa kifikra na kiutamaduni. Madai ya kutokujitenga na ulimwengu yaliwahi pia kutolewa na Crystal (2003) akidai kwamba nyenzo za tafsiri na ukalimani haziwezi kuyasaidia kwa ufanisi makundi changamani zaidi kiisimu yanapokutana kwa ajili ya mijadala ya kimataifa. Alisisitiza kuwa na lugha moja ya ulimwengu ili kurahisisha mawasiliano na akapendekeza kuwa Kiingereza ni lugha mwafaka yenye sifa hiyo. Kabla ya kutoa ufafanuzi zaidi, inafaa kurejelea maelezo ya mchangiaji mwingine ambaye aliandika:

> Hivi dunia ya leo bado tunawaza lugha ya Kiingereza kuwa ni ya Waingereza? Ibakie historia kwamba lugha chimbuko lake ni huko! *Anyway* [haijalishi], tunataka watu wafanye uvumbuzi sawa, lakini uvumbuzi usioendelezwa ni kazi bure, wenye mamlaka waelekeze nguvu kwa vijana, wana vingi vizuri, wengine wamevumbulia kwa lugha ya Kisukuma!
> **Chanzo:** *WhatsApp* UDASA-MUCE, tarehe 10 Juni 2022

Mtazamo unaojitokeza katika madondoo hayo hapo juu unachukulia kuwa kutumia Kiswahili kufundishia ni kuondoa msisitizo wa lugha ya Kiingereza. Kwa mujibu wa Lupogo (2014), kudhani kwamba kutumia lugha ya kigeni kufundishia kunakuza umilisi wa lugha ni upotoshaji. Hii ni kwa sababu walimu ambao hawana misingi ya somo la Kiingereza wanazalisha malighafi za lugha hiyo zenye

dosari kwa wanafunzi. Dosari hizo zinaweza kuepukwa kwa kutumia walimu wenye ujuzi wa kutosha katika ufundishaji wa lugha za kigeni. Mawazo haya ni sawa na ya Qorro (2023) anayesisitiza kwamba kudorora kwa lugha ya Kiingereza katika shule za sekondari kunatokana na kutokuwa na malengo yaliyo bayana kuhusu matumizi ya Kiingereza. Matokeo yake wanafunzi wanasikia Kiingereza kisicho fasaha kwa muda mrefu zaidi kuliko muda unaotumiwa na walimu wenye sifa za kufundisha Kiingereza fasaha.

Kimsingi, jamii makini haiwezi kuandaa mitaala ya elimu ambayo msisitizo wake ni kujua lugha ya kigeni. Fasili ya lugha ya kigeni ni sawa na ile ya Qorro (2023) kwamba inatumika katika mazingira maalumu anapotokea mgeni ambaye hafahamu lugha ya jamii husika. Mitaala makini inapaswa kusisitiza maarifa na ujuzi unaohitajika kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za maisha ya jamii. Motshekga (2022) ameonya tabia ya nchi za Kiafrika kutunga mitihani inayopima umilisi wa lugha za kigeni zinazotumika kufundishia badala ya maarifa na ujuzi unaohitajika kwa maendeleo ya watu. Meena (2023) amekemea bayana kwamba upimaji unakuwa na shaka pale inapotumika lugha ambayo mtahiniwa haifahamu vizuri. Kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda utamaduni na kukuza fikra huru na tunduizi kama ilivyoelezwa katika tafiti nyinginezo ni kwamba lugha ya Kiswahili inafaa kufundishia katika ngazi zote wakati mikakati inawekwa kwa ajili ya kuimarisha ufundishaji wa lugha ya Kiingereza na lugha zingine za kigeni nchini Tanzania.

Uhakiki wa maudhui ya sehemu hii unadhihirisha mwangwi wa maarifa yaliyohodhiwa na mifumo ya kikoloni. Ni vigumu kwa Tanzania kujitegemea kwa kufanya shughuli zake chini ya ukoloni wa lugha, utamaduni na fikra ambazo zinatokana na kiunzi kilichobuniwa kimkakati kuzifanya jamii kuwa dhalili. Mazrui (1997) anasisitza kwamba lugha za kikoloni zinazotumika kuzalisha wasomi wa Kiafrika ni chanzo kikubwa cha ukolonia. Kwa mujibu wa Kazeen na Suleiman (2020), sera ya lugha nchini Nigeria inapendelea lugha ya Kiingereza na kuifanya kuwa bora zaidi kuliko lugha za wazawa.

Matokeo ya hali hiyo ni uwiano mdogo baina ya maarifa asilia na maarifa ya kimataifa katika mitaala ya elimu. Hali ilivyo nchini Nigeria inawiana na ya Tanzania. Qorro (2023) anataja madhara ya kufundisha kwa lugha ya kigeni kuwa ni kukatika kwa mawasiliano kati ya wasomi na jamii pana wanayotokana nayo. Elimu nchini Tanzania haikuzi maarifa asilia na kundi la wasomi limeendelea kuishi katika ukimbizi wa kisaikolojia. Elimu haijengi ari ya kujitegemea kwa sababu wanafunzi hawapati hisia ya ubunifu na hawawezi kuona rasilimali zilizopo katika jamii zao. Kutumia lugha ya kigeni kunaifanya Tanzania kuendelea kutoa maarifa bila ujuzi wa kuwafanya watu wajitegemee katika mazingira yao.

### 3.3 Kiswahili Hakiwezi Kufumbata Maarifa ya Sayansi

Kuna mtazamo kwamba kuna lugha mahususi zilizojaliwa uwezo wa kuvumbua na kufumbata maarifa ya sayansi. Inadhaniwa kuwa maarifa hayo hayawezi kuelezwa

kwa lugha nyingine kama ilivyo Kiswahili kwa sababu hazikujaliwa uwezo huo. Mchangiaji mmojawapo alikuwa na haya ya kueleza:

> … nyie mnawaza kujifunza fizikia kwa Kiswahili kweli au ndio tutaanza kukariri upya. … Tuache kuifanya elimu yetu kuwa ya majaribio…. Embu wamuite daktari halafu alivyovisomea viwe kwa Kiswahili kama kuna kitu anaweza kufanya. So mtu kamaliza *degree* [shahada] yake hapa Tanzania akitaka kuendelea kusoma nje ya nchi eti akaanze tena kujifunza Kingereza. *Shame upon them. I would advice them to use english as language of teaching for all subjects except* [aibu yao. Ningewashauri kutumia Kiingereza kuwa lugha ya kufundishia katika ngazi zote isipokuwa ….] Kiswahili.
>
> **Chanzo:** *WhatsApp* UDASA-MUCE, tarehe 10 Juni 2022

Maoni hayo yanatofautiana na ya Mosha (2023) na Mutembei (2023) ambao wanakubaliana kwamba lugha ya Kiswahili inaendana na wakati na ina msamiati nyumbufu kama itapewa nafasi ya kutumika. Kinachojitokeza katika dondoo hilo ni athari za moja kwa moja za kasumba ya utegemezi kama anavyoeleza Moyo (2009) kwamba kwenye kiini cha Mwafrika, kuna fikra ya kutoweza kupata maendeleo na kuboresha maisha yake bila msaada wa kigeni. Akili zinazoshadidia utegemezi kama suluhisho lisilo na mbadala zimezingirwa na mifumohodhi ya fikra ambayo inapaswa kuondolewa kwa nguvu. Cystal (2003) anasisitiza kwamba kuondoa ukoloni na athari zake akilini ni hatua ya kwanza na muhimu ya kubadili mitazamo kuhusu ulimwengu katika nchi zilizotawaliwa.

Maarifa yasichukuliwe kuwa ni mali ya baadhi ya lugha na kupuuza mantiki kwamba lugha ni nyenzo ya kubebea maarifa ambayo kimsingi hayamilikiwi na lugha mahususi. Katika mijadala kuhusu lugha ya kufundishia shuleni, baadhi ya watu wanataka kuhakikishiwa kwamba kila istilahi ya kifizikia tayari ina msamiati unaowiana nao katika lugha ya Kiswahili. Mtazamo kama huo unatokana na kutofahamu kaida za kiisimujamii kwamba lugha hukua baada ya kupewa majukumu.

### 3.4 Uchumi Duni Unaathiri Matumizi ya Kiswahili katika Elimu

Lugha inayofungamana na jamii yenye uchumi duni inakuwa katika nafasi finyu ya kuthaminiwa na kutumika kwa matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufundishia shuleni. Mchangiaji mmojawapo alikuwa na maoni kwamba mjadala kuhusu lugha ya kufundishia unapaswa kutanguliwa na hatua stahiki za kuondoa umaskini. Huyu aliandika:

> …nani aliyetuloga kuwa lugha ni tatizo la kutukwamisha maendeleo yetu? Iga ufe. Wenzetu walitumia lugha zao kama silaha huku wakiwa na uchumi imara. Huwezi kuwa na lugha imara wakati unatembeza bakuli. Mjapani au

> Mchina anatumia lugha yake kwenye *innovations* [ubunifu] zake na hatuna ubavu wa kumwambia akutengenezee gari aweke manual [mwongozo wa mtumiaji] ya Kiswahili.
> **Chanzo:** *WhatsApp* UDASA-MUCE, tarehe 10 Juni 2022

Kimsingi, maelezo hayo yanamaanisha kuwa udhalili wa lugha ya Kiswahili ni taswira ya umaskini wa watumiaji wake, hivyo, ni vigumu kuikuza kwa ajili ya kufundishia. Suala la umaskini kuathiri ukuaji wa lugha limewahi kuelezwa na Crystal (2003) kwamba nguvu ya lugha haitokani na sifa zake za kiisimu bali inapata nguvu kutoka kwa watumiaji wake. Watumiaji wa lugha wanapokuwa dhaifu kutokana na uchumi duni, lugha na utamaduni wao hubezwa na kutwezwa. Katika dhana ya ubeberu wa kiisimu, uchumi una nafasi kubwa ya kuendeleza ukoloni wa lugha (Phillipson, 1992). Kwa msingi huo, tatizo si lugha ya Kiswahili kushindwa kukidhi haja ya matumizi, bali kukosekana kwa uchumi thabiti ambao ni muhimu katika kuimarisha uhuru wa kujitegemea kifikra, kujichagulia na kukuza rasilimali zilizopo nchini ikiwa ni pamoja na lugha.

Hata hivyo, uamuzi wa lugha kihadhi ni utashi wa kisiasa. Utashi huo ni muhimu katika kupanga rasilimali kiasi gani ziwekezwe kwenye ukuzaji wa lugha ili ikidhi mahitaji ya matumizi. Mtazamo huu unawiana na matokeo ya utafiti wa Tibategeza na Du Plessis (2018) uliobaini kuwa juhudi za kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa ya kufundishia katika ngazi zote za elimu zinakwamishwa na utashi duni wa kisiasa. Kwa mujibu wa kiunzi cha Ubadaukoloni, utashi duni wa kisiasa unaweza kufasiliwa kuwa ni matokeo ya usukuku wa ukolonia wa maarifa miongoni mwa watu waliopewa dhamana ya kufanya maamuzi kuhusu lugha. Katika mjadala kuhusu ubora wa elimu nchini, nafasi ya lugha ya wazawa haiwezi kupita bila kusailiwa kwa sababu kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya matokeo mabaya na matumizi ya lugha ya kigeni kufundishia elimu ya juu (Mekhize na Balfour, 2017). Kwa mujibu wa Vuzo (2019), lugha inayofaa kufundishia ni ile ambayo inafahamika vizuri na isiyomtenganisha mwanafunzi na mazingira ya utamaduni wake. Maelezo hayo yanawiana na kiunzi kilichowekwa na Benki ya Dunia kama mwongozo wa kuhakiki ubora wa elimu.

Kiunzi hicho kinasisitiza umuhimu wa elimu kuzingatia utamaduni wa jamii husika. Hali ilivyo nchini Tanzania, elimu inayotolewa haimwandai mwanafunzi kukabiliana na mazingira yake kutokana na matumizi ya lugha ya kigeni. Kwa mujibu wa Senkoro (2008), kutumia lugha isiyofahamika vizuri kwa wajifunzaji ni sawa na kubadili malengo ya elimu. Kisaikolojia, kuna ushahidi kwamba kiwango cha kujikubali kinaukilia kiwango cha mafanikio ambayo mtu au jamii inaweza kuyapata katika jitihada zake za kujitafutia nusura (Kapinga na Mbwiga, 2021). Kwa hiyo, wasomi wazawa kuikataa lugha yao ni kujikataa kuwapo kwao na kukwamisha maendeleo yao.

### 3.5 Umuhimu wa Kuondokana na Utumwa wa Lugha na Utamaduni

Baadhi ya wanazuoni walieleza kwamba hakuna sababu ya kuendelea kutumia lugha na tamaduni za kigeni katika taifa ambalo lina lugha na utambulisho wake. Baadhi ya wachangiaji walitoa maoni yaliyoonesha kukerwa na matumizi ya lugha za kigeni katika mawasiliano na mfumo wa elimu kiasi cha kufanywa dhalili. Mchangiaji mmojawapo alionesha hisia kali na kushangazwa kwa nini tuendelee kutukuza lugha na utamaduni wa kigeni, aliandika:

> Kwani hatuna lugha zetu? Au hapa pamekuwa Uingereza? Au sisi hatuna utamaduni wetu wa kujivunia na kuuendeleza na kuukuza katika elimu? Kwanza hao walimu wa kufundisha hiyo lugha isiyo yetu tunao? Au gharama za kuwakodi tunaweza kuzimudu? Na kwa nini tuende huko?
>
> **Chanzo:** *Whatspap* UDASA-MUCE, tarehe 10 Juni 2022

Maoni hayo yanaonesha kutoridhishwa na utamaduni unaoelekea kumtenga mtu na mazingira yake kupitia lugha na masuala mengine yanayowatenga watu na mazingira yao. Kutengwa na mazingira kunawafanya watu wasipate hisia za kweli za kujitegemea kifikra na kiuchumi. Elimu ni zana ya itikadi ya dola, hivyo, lugha inayotumika ina nafasi kubwa ya kutoa mwelekeo wa jinsi fikra zinavyoundwa na kuzalishwa katika jamii husika. Kutumia lugha za kigeni ni kueneza itikadi za kigeni na kubadili malengo ya elimu (Senkoro, 2008). Katika hali kama hiyo, vyuo vikuu nchini Tanzania haviwezi kuwafanya wanafunzi wauone ulimwengu kwa macho halisi huku wakisaidiwa kuchunguza kwa makini maadili ya kitamaduni, kuwasilisha maadili chanya katika mikutano ya kiulimwengu na kukataa maadili hasi ya kigeni. Kauli maarufu katika dhana ya Ubuntu kwamba “Nipo kwa sababu upo, na kwa sababu upo, basi nipo” inawataka Waafrika kushiriki ubinadamu wao bila kulazimika kushiriki furaha na huzuni za wengine kwa gharama za kufuta kuwapo kwao (Bolden, 2014).

Kutumia lugha ya kigeni kurithisha amali za jamii ni kushiriki furaha na huzuni za watu wengine kwa kufuta kuwapo kwao kama jamii huru. Katika mwelekeo wa kukataa utumwa wa lugha na utamaduni, baadhi ya wanazuoni walielekeza lawama kwa serikali kwa kushindwa kufanya uamuzi wa kuruhusu Kiswahili kitumike katika ngazi zote za elimu kwa kuandika:

> *Debate* [mdahalo] hii ingeshaisha bwana. Kinachokosekana tu ni *'political will'* [utashi wa kisiasa] *Political Will* [utashi wa kisiasa] kwa upande wa Tanzania inategemea sana uelekeo wa upepo na sio uzito wa hoja. Bado wanaangalia kujua upepo unavuma kuelekea wapi zaidi. Watakuwa wanaogopa mabeberu na lugha yao. Ila ushahidi upo wazi juu ya lugha

> inayopaswa kutumika kufundishia. Wasome matokeo ya tafiti za mradi wa LOITASA, uliosimamiwa na Prof. Birgit Brock-Utne na Prof. Martha Quoro.
>
> **Chanzo:** *WhatsApp* UDASA-MUCE, tarehe 10 Juni 2022

Maoni hayo yanaonesha kwamba hakuna utashi wa dhati wa kutumia Kiswahili. Moshi (2023) ameweka bayana kwamba katika dira zote za maendeleo zilizoandaliwa baada ya Azimio la Arusha, hakuna dira iliyowahi kutaja bayana kwamba Kiswahili kitakuwa lugha ya kufundishia licha ya umuhimu wake katika kuleta maendeleo. Kukosekana kwa mikakati thabiti ya kutekeleza Sera ya Elimu ya 2014 ni ushahidi mwingine wa kukosekana kwa utashi wa kisiasa. Katika kiunzi cha Ubadaukoloni mamlaka zinaogopa kuondoa Kiingereza kwenye mfumo wa elimu kwa kuhofia hasira za wakoloni wanaopenda kuona lugha yao ya Kiingereza inaendelea kutukuzwa. Brock-Utne (2015) anaeleza bayana kwamba uteuzi wa lugha ya kufundishia ni eneo ambalo linazua taharuki kubwa miongoni mwa watawala wa zamani wa nchi za Kiafrika wakiwa wanahaha kuendelea kuimarisha lugha zao katika makoloni hayo ya zamani. Kwa hiyo, maamuzi yanayotekelezwa ni matokeo ya ushindi wa Ubeberu wa Kiisimu ambao ni sehemu ya Ubeberu wa Kiulimwengu.

### 3.6 Mfumo wa Uwililugha katika Elimu kama Hatua ya Mpito

Baadhi ya wanazuoni wanakubali umuhimu wa kubadili lugha ya kufundishia kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili katika ngazi zote za elimu. Hata hivyo, wana mtazamo kwamba mfumo wa elimu nchini Tanzania utumie lugha mbili, yaani Kiswahili na Kiingereza katika ngazi zote za elimu kama hatua ya mpito kuelekea kwenye matumizi ya lugha ya Kiswahili peke yake. Kuhusiana na mtazamo huo, mchangiaji mmojawapo alikuwa na haya ya kueleza:

> ...tu*adopt* [tutumie] *"Biligual model"* [modeli ya uwililugha] *as a model of teaching at secondary school* [kama modeli ya kufundishia katika shule za sekondari]. Na hii naikubali kama hatua ya kuanza kuelekea kwenye matumizi ya lugha yetu adhimu, nzuri, Kiswahili kama lugha ya kujifunzia, kuchakata maarifa na ubunifu katika kufundisha masomo ya elimu yetu. *Then* [kisha] wakati tuna *adopt* [anza kutumia] hiyo *model* [modeli] tutahitajika tu-*invest* [tuwekeze] zaidi katika maandalizi ya mwalimu wa Kiingereza kuanzia shule za msingi ambapo msingi wa lugha kama somo unatakiwa kujengwa. Vyuo vinavyoandaa mwalimu au walimu wa masomo mengine navyo mitaala yake iboreshwe ili vitoe walimu watakaokidhi mahitaji yaliyopo shuleni. Hata hivyo, tunaposema Kiingereza kisitumike sekondari kama lugha pekee ya kufundishia hatumaanishi kuwa ni muarobani wa matatizo tuliyonayo ya elimu ….
>
> **Chanzo:** *WhatsApp* UDASA-MUCE, tarehe 10 Juni 2022

Mchangiaji wa mjadala anaonesha msimamo kuwa Kiswahili kitumike katika ngazi zote za elimu. Kwa hatua ya kwanza anapendekeza kuwe na uwililugha katika elimu kabla ya hatua ya kukiacha Kiswahili kitumike peke yake. Mtazamo wa kuwa na uwililugha katika elimu unawiana na ule wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Tanzania ya mwaka 2014 ambao haukutekelezwa. Katika sera hiyo, sawa na maoni ya dondoo ya hapo juu modeli yenyewe ya uwililugha katika elimu haiko wazi. Kwa mfano, kunaweza kuwa na shule tofauti ambapo baadhi zinafundisha kwa Kiswahili na zingine zinafundisha kwa Kiingereza kama inavyofanyika kwa sasa. Pia, lugha mbili zinaweza kutumika kwa kukamilishana ndani ya darasa moja kwa wakati mmoja au ndani ya shule moja kunaweza kuwa na madarasa yanayotofautiana lugha ya kufundishia. Kwa hiyo, maoni yake ni mazuri lakini inafaa kuchunguza modeli nyingi iwezekanavyo kabla ya kuyaunga mkono.

Hata hivyo, mchangiaji wa mjadala hakueleza kwa nini Kiswahili hakiwezi kutumika peke yake kuanzia hatua ya kwanza bila kipindi cha mpito cha uwililugha. Kwa mujibu wa kiunzi cha Ubadaukoloni, inaonesha bado kuna wasiwasi mkubwa kuhusu uwezo wa lugha ya Kiswahili kuhimili maarifa katika ulimwengu changamani. Wasiwasi anaouonesha unayafanya maoni yake yafanane kwa kiasi na maoni ya wanazuoni wengine wanaokataa kabisa kukiondoa Kiingereza katika mfumo wa elimu Tanzania. Wasiwasi unaodhihirika katika maoni hayo ni matokeo ya juhudi kubwa zinazofanywa na mifumo ya kibeberu katika kuhakikisha utawala wa kiisimu unaendelea katika makoloni yao ya zamani. Mchangiaji mwingine ingawa alikuwa hagusii suala la elimu moja kwa moja alikuwa na maoni kwamba kuzifahamu lugha zaidi ya moja ni faida kutokana na kuwapo katika ulimwengu wenye wingilugha. Maoni yake kuhusu umuhimu wa wingilugha yamekitwa katika matumizi ya lugha kibiashara. Naye aliandika:

> ... kwangu mimi kufahamu lugha zaidi ya moja ni faida *"credit"*. Kwenye maisha hasa ya kibiashara n.k. …vivyo hivyo kwenye lugha za mataifa mbalimbali ni vizuri tukajua hata kidogo, tukifika na ajenda zetu watatuelewa zaidi na watajua ni wenzetu lakini tusilowee huko na kusahau "*kupromote"* [kukuza] lugha yetu na kutekeleza ajenda zetu. Ahsante.
>
> **Chanzo:** *WhatsApp* UDASA-MUCE, tarehe 10 Juni 2022

Maoni hayo yanatupatia picha kwamba kufahamu lugha zaidi ya moja ni muhimu kwa mawasiliano katika dunia ambayo imejaa jamii zenye usuli tofauti wa kiisimu. Pamoja na umuhimu huo, inafaa kusisitiza hapa kwamba si kila lugha tunayotaka kuifahamu kwa ajili ya mawasiliano ya kibiashara lazima itumike kwenye mfumo wa elimu. Makala hii inasisitiza umuhimu wa Kiingereza kufundishwa kikamilifu sanjari na lugha zingine za kigeni ili kukidhi mahitaji ya lugha za kigeni kwa Watanzania kulingana na mahitaji yao. Ifahamike kuwa

miktadha mingi ya matumizi ya lugha ni changamani kiisimu na si wafanyabiashara wote wa Tanzania wanafanya miamala na nchi za wazungumzaji wa Kiingereza peke yake. Hata hivyo, harakati za kujiondoa katika kile ambacho Soyinka (2009) anakiita ubeberu mpya lazima ziendelee kwa ajili ya ukombozi wa fikra, utu na ujumi wa mtu mweusi ulimwenguni.

## 4.0 Hitimisho na Mapendekezo

Mjadala kuhusu lugha ya kufundishia shuleni nchini Tanzania ni wa muda mrefu. Maoni yanayotolewa kila mjadala unapoibuka yanakosa urazini huru kwa sababu ya usukuku wa ukolonia. Watungasera na wasomi wamekumbwa na kile kilichoelezwa na Nagarajan (2006) kama 'ukimbizi wa kisaikolojia'. Wanazuoni wanapaswa kurejeshwa kutoka ukimbizini ili wathamini lugha na utamaduni wao. Pendekezo la makala hii ni kwamba hatua za kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutumia lugha zao au lugha za mawasiliano mapana kama vile Kiswahili katika mfumo wa elimu zianzie kwa wasomi. Vilevile, kuna umuhimu wa serikali kutumia mapendekezo ya kisera yanayotokana na tafiti na kuhakikisha utashi wa kisiasa unalenga masilahi mapana ya taifa.

## Marejeleo


Bokamba, E.G. (2011). "Ukolonia in African Language Policies and Practices". Katika E.G. Bokamba (Mh.), *Selected Proceedings of the 40th Annual Conference on African Linguistics.* Someville: Cascadilla Proceedings Project. Kur. 146-167.

Bolden, R. (2014). "Ubuntu". Katika D. Coghlan na M. Brydon (Wah.), *Encyclopedia of Action Research*. London: Sage. Kur. 1-8.

Brock-Utne, B. (2015). "Language in Education Policies and Practices in Africa with a Special Focus on Tanzania and South Africa". Katika J. Zajda (Mh.), *Second Handbook on Globalization, Education and Policy Research.* Oslo: Springer Science & Business Media. Kur. 615-631.

Crystal, D. (2003). *English as a global language*. Cape Town: Cambridge University Press.

Fanon, F. (1952). *Black Skin, White Masks*. London: Routledge.

Fanon, F. (1961). *The Wretched of the Earth*. New York: Grove Press.

Fussy, D.S. (2022). "Use of Research Evidence in the Policy Domain: A Best-evidence Synthesis of Social Science Research in Africa, Asia, and Latin America". *International Social Science Journal.* 72 (246): 1181 - 1194.

Kapinga, O.S. na Aloni, M. (2023). Measuring Levels of Self-esteem of Students with Visual Impairments in Regular Schools in Tanzania. *British Journal of Visual Impairment.* 41(2), 388-399.

Kawonga, G.A. (2023). "Mtazamo Mpya kuhusu Lugha ya Kiswahili na Elimu ya Juu nchini Tanzania". Katika D. S. Fussy, H. I. Hassan, J. A. Moshi, O. S. Kapinga, O. J. Magava, S. T. Mkimbili na V. J. Cosmas (Wah.),

*Proceedings of the First International Conference on Contemporary Issues in Education: Linking Research and Practices*. Dar es Salaam: DUP. Kur. 126-143.

Lupogo, I. (2014). "Language of Instruction: A Challenge for Secondary Schools and Tertiary Institutions in Implementing VET in Tanzania". *Journal of Education and Entrepreneurial Research.* 1(3): 26-30.

Lyimo, T. (2022). "Let's Harmonize Curricula and Syllabuses to Improve Quality of our Education." *The Gurdian.* 29 Julai 2022. Uk. 9.

Makweta, J. (2012). "Ubabaishaji wa Viongozi ni Kikwazo kwa Elimu ya Tanzania". Katika E. Missoki (Mh.), *Hali ya Elimu Tanzania: Miaka 50 Baada ya Uhuru, Tufanye nini Tuweze Kusonga Mbele*? Dar es Salaam: HakiElimu. Kur. 8-12.

Mazrui, A. (1997). "The World Bank, the Language Question and the Future of African Education". *Race and Class.* 38(3): 36-47.

Meena, W.E. (2023). "Tafakuri ya Jumla: Kiswahili Kitumike Kuimarisha Usawa katika Kujifunza na Upimaji". Katika W. E. Meena na J. Kalage (Wah.), *Lugha ya Kufundishia Kikwazo cha Usawa katika Kujifunza na Upimaji Tanzania: Kiswahili Kichocheo cha Kukuza Fikra Tunduizi na Ubunifu.* Dar es Salaam: HakiElimu. Kur. 6-11.

Meissner, W.W. (2008). "The Role of Language in the Development of the Self II: Thoughts and Words". *Psychoanalytic Psychology*. 25 (2): 220-241.

Mekhize, D. na Balfour, R. (2017). "Language Rights in Education in South Africa". *South African Journal of Higher Education.* 31(6): 13-150.

Mosha, H. (2018). "The State and Quality of Education in Tanzania: A Reflection". *Papers in Education and Development.* (31).

Moshi, H.P.B. (2023). "Kiswahili ni Lugha ya Taifa: Kwa nini sio Lugha ya Kufundishia?" Katika W.E. Meena na J. Kalage (Wah.), *Lugha ya Kufundishia Kikwazo cha Usawa katika Kujifunza na Upimaji Tanzania: Kiswahili Kichocheo cha Kukuza Fikra Tunduizi na Ubunifu.* Dar es Salaam: HakiElimu. Kur. 25-29.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Mutembei, A.K. (2023). "Gogo la Mti Lijapowekwa Mtoni Miaka 100 Haliwezi Kugeuka kuwa Mamba: Tutumie Kiswahili kuwa Lugha ya Utambulisho na Kukuza Maarifa". Katika W. E. Meena na J. Kalage (Wah.), *Lugha ya Kufundishia Kikwazo cha Usawa katika Kujifunza na Upimaji Tanzania: Kiswahili Kichocheo cha Kukuza Fikra Tunduizi na Ubunifu.* Dar es Salaam: HakiElimu. Kur. 12-24.

Nagarajan, M.S. (2006). *English Literary Criticism and Theory: An Introductory History*. New Delhi: Orient Blackswan.

Nayar, P.K. (2010). *Contemporary Literary and Cultural Theory from Structuralism to Ecocriticism*. Noida: Pearson.

Ochieng, H.K. na Yeonsung, C. (2021). “Political Economy of Education: Assessing Institutional and Structural Constraints to Quality and Access to Education Opportunities in Tanzania”. *SAGE Open*. 11 (3): 21582440211047204.

Phillipson, R. (1992). *Linguistic Imperialism*. London: Oxford University Press.

Phillipson, R. (2003). *English-only Europe? Challenging Language Policy*. London: Routledge.

Phillipson, R. (1997). “Realities and Myths of Linguistic Imperialism”. *Journal of Multilingualism and Multiculturalism Development.* 18 (3): 238-248.

Qorro, M. (2023). “Kuboresha Ufundishaji wa Kiingereza katika Shule za Sekondari Tanzania: Umuhimu wa Kuzingatia Maelekezo ya Nadhari.” Katika W. E. Meena na J. Kalage (Wah.), *Lugha ya Kufundishia Kikwazo cha Usawa katika Kujifunza na Upimaji Tanzania: Kiswahili Kichocheo cha Kukuza Fikra Tunduizi na Ubunifu.* Dar es Salaam: HakiElimu. Kur. 30-45.

Qorro, M.A.S. (2009). “Parents and Policy-makers Insistence on Foreign Language as a Medium of Education in Africa: Restricted Access to Quality Education for Whose Benefit?” Katika Brock-Utne na I. Skahum (Wah.), *Language and Education in Africa: A Comparative and Transdisciplinary Analysis*. Oxford: Symposium. Kur. 241 - 267.

Qorro, M. A. S. (2013). “Language of Instruction in Tanzania: Why is Research Findings not Heeded?” *International Review of Education.* 59 (1): 29-45.

R’boul, H. (2022). “English Medium Instruction in Moroccan Universities: Implications for Multilingualism, Linguistic Dependency and Epistemic Justice”. *Journal of Multilingual and Multicultural Development. 45*(7): 2770-2784.

Rwantabagu, H. (2011). “Tradition, Globalization and Language Dilemma in Education: African Option for the 21st Century”. *International Review of Education.* 457-475.

Sa’di, A.H. (2021). “Orientalism in a Globalised World: Said in the Twenty-First Century”. *Third World Quarterly.* 42 (11): 2505-2520.

Said, E. W. (1978). *Orientalism*. Toronto: Pantheon Books.

Soyinka, W. (2009). “New Imperialism”. Katika I. Shivji (Mh.), *Reimagining Pan-Africanism: Distinguished Mwalimu Nyerere Lecture Series 2009-2013*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers. Kur. 5-50.

Telli, G. (2014). “The Language of Instruction Issue in Tanzania: Pertinent Determining Factors and Perception of Education Stakeholders”. *Academic Journals.* 5 (1): 9 - 16.

wa Thiong'o, N. (1986). *Decolonizing the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Nairobi: Heinemann.

Tibategeza, E. R. na du Plessis, T. (2018). "The Prospects of Kiswahili as a Medium of Instruction in the Tanzanian Education and Training Policy". *Journal of Language and Education.* 4 (3): 88 - 98.

Vuzo, M. (2018). "Towards Achieving the Sustainable Development Goals: Revisiting Language of Instruction in Tanzania Secondary Schools". *International Review of Education.* 64: 803-822.

Vuzo, M. (2019). "Implementation of Sustainable Language Education in the Tanzanian Context: A critical Review". *African Education Indices.* 11: 2-21.

World Bank (2014). "The Six A's of Quality Education". The Worldbank Blogs. https://blogs.worldbank.org/education/six-s-quality-education